



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HMM/P.40/VOL.XII/97

Tarehe: 24 Mei, 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Manispaa ya Musoma inakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa wananchi wenye sifa zinazotakiwa ili kujaza nafasi zifuatazo:-

1. Katibu Muhtasi Daraja III – Nafasi 4

1.1 Sifa za Mwombaji

Awe amehitimu kidato cha IV na kuhudhuria Mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu. Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno **80** kwa dakika moja na awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika programu za Window, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

1.2 Majukumu ya Kazi

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa wakati unaohitajika.

- Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majadala, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.

2. Dereva Daraja II - NAFASI 4

2.1 Sifa za Mwombaji

- Kuajiriwa mwenye cheti cha kidato cha Nne (Form **IV**) na Leseni daraja la **E** au **“C”** ya uendeshaji magari ambayo amefanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali. Waombaji wenye cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

2.2 Majukumu ya Kazi ni pamoja na:-

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
- Kutunza na kuandika daftari la safari “Log-book” kwa safari zote,
- Kufanya usafi wa gari na
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake

2.3 Mshahara

Utakuwa katika ngazi za mishahara ya Serikali yaani **TGS B**

3 MTENDAJI WA MTAA DARAJA III - NAFASI 9

3.1 Sifa za Mwombaji

- ❖ Awe na Umri wa miaka **18 – 40**.
- ❖ Awe na Elimu ya Kidato cha nne au sita.

- ❖ Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada (cheti) katika mojawapo ya fani zifuatazo:- Utawala, Sheria,Elimu ya Jamii,Usimamizi wa Fedha,Maendeleo ya Jamii au Sayansi ya Sanaa kutoka Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

3.2 Majukumu ya Kazi ni pamoja na kuwa:-

- ❖ Katibu wa Kamati ya Mtaa.
- ❖ Mtendaji Mkuu wa Mtaa
- ❖ Mratibu wa utekelezaji wa Sera na sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa.
- ❖ Mshauri wa Kamati ya mtaa kuhusu Mipango ya Maendeleo katika Mtaa
- ❖ Msimamizi wa utekelezaji wa sheria ndogo pamoja na sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa.
- ❖ Mshauri wa Kamati ya mtaa kuhusu masuala ya ulinzi na usalama.
- ❖ Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umasikini katika Mtaa.
- ❖ Msimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.
- ❖ Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa mtaa na;
- ❖ Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

3.3 Mshahara

Ngazi ya mshahara ya **TGS B**

4. Mhudumu wa Jikoni/Mess Daraja la II (Kitchen/Mess Attendant) - Nafasi 3

4.1 Sifa za Mwombaji

- ❖ Awe na Umri wa miaka **18 – 40**.
- ❖ Awe na Elimu ya Kidato cha nne

4.2 Majukumu ya Kazi ni pamoja na kuwa:-

- ❖ Kusafisha Vyombo vya kupikia
- ❖ Kusafisha Vyombo vya kulia chakula
- ❖ Kusafisha Meza itumiwayo kwa kulia chakula
- ❖ Kuwatayarishia Wapishi/Waandazi vifaa vya Mpishi na Mezani
- ❖ Kusafisha maeneo ya kulia chakula na kupikia
- ❖ Kuwasaidizi Wasaidizi na Wapishi

3.3 Mshahara

Ngazi ya mshahara ya **TGOS A**

5. Dereva wa Mashua/Vivuko Daraja la II - Nafasi 2

5.1 Sifa za Mwombaji

- ❖ Awe na Umri wa miaka **18 – 40**.
- ❖ Awe na Elimu ya Kidato cha nne
- ❖ Awe na ujuzi wa kuendesha na kutunza Mashua/Kivuko uliothibitishwa na Chuo cha Dar Es Salaam Marine Institute au Chuo kingine chochote kinachotambuliwa na Serikali kwa muda usiopungua miaka miwili; na waliofuzu mafunzo ya miezi sifa uokoaji wa maisha majini, kuogelea na kupanga watu na magari kwenye mashua/vivuko

5.2 Majukumu ya Kazi ni pamoja na kuwa:-

- ❖ Kufunga na kufunga kamba za mashua/kivuko
- ❖ Kuchunga usalama wa abiria na magari yaliyomo ndani ya mashua/vivuko
- ❖ Kupanga abiria au magari kwenye mashua/vivuko
- ❖ Kuendesha na kuongoza mashua/kivuko
- ❖ Kutunza daftari za safari ya mashua/vivuko
- ❖ Kuhakikisha kwamba injini za kivuko zipo katika hali nzuri ya kufanya kazi
- ❖ Kuangalia mafuta na vyombo vingine vya kufanyia kazi

Mshahara

Ngazi ya mshahara ya **TGOS A**

Masharti:

- Waombaji wote wawe na umri usiozidi miaka **45**
- Maombi yaandikwe kwa mkono na kuambatishwa
 - Cheti cha kuzaliwa
 - Maelezo binafsi(**CV**)
 - Nakala za vyeti vya kuhitimu Elimu ya Msingi, kidato cha nne au sita, cheti cha Taaluma.
 - Picha mbili ndogo "Passport Size", anuani na namba ya simu
 - **Testimonials, provisional results, Result Slip ya Kidato cha IV na VI HAVITAKUBALIWA**
 - Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika yaani **NECTA** na **NACTE** na taarifa ya ithibati iambatanishwe kwenye maombi.

NB: Maombi yasiyozingatia masharti tajwa hapo juu hayatashughulikiwa.

Namna ya kutuma maombi.

Maombi yatumwe kwa:-

***MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA,
S.L.P. 194,
MUSOMA***

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 06 Juni, 2022

Limetolewa na:-

Bosco O. Ndunguru
**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
MUSOMA**